


HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

Barua pepe:info@nsimbodc.go.tz
Tovuti:www.nsimbodc.go.tz



S.L.P 688

MPANDA

Press No: NDC/ICPRU/Press no.09

17 Aprili 2018

TAARIFA KWA UMMA YAH: MAPOKEZI YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA KWA MWAKA 2018 HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Bw.Mwailwa Smith Pangani**,anawatangazia Wananchi wote kuwa mapokezi ya mbio za mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa Mwaka 2018 katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo yatafanyika **Tarehe 3/05/2018** saa mbili kamili asubuhi katika Kijiji cha Ikondamoyo kilichopo katika Kata ya Uruwira Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Hivyo wananchi wote mnaombwa kutoa ushirikiano wa dhati kuanzia mapokezi ya mbio za Mwenge wa Uhuru ikiwa ni pamoja na kujitokeza pembezoni mwa barabara ambamo mwenge wa Uhuru utapita, pamoja na kujitokeza kwa wingi katika Mkesho wa Mwenge katika Kata ya Kanoge eneo la Uwanja wa Mpira Kanoge Laini kwa ajili ya Kukesha pamoja na Mwenge wa Uhuru.

Aidha kutakuwa na mkesho utakaoambatana na burudani ya ngoma,nyimbo za kwaya na muziki zitakazotolewa na Wasanii mbalimbali na Vikundi vya ngoma vya asili kwa ajili ya maandalizi ya kuupokea Mwenge wa Uhuru katika Kijiji cha Ikondamoyo Kata ya Uruwira,utakaoanza kuanzia Aprili 2 2018 saa 12 kamili jioni mpaka Asubuhi.

Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa mwaka 2018 zinabeba ujumbe unaosema **“Elimu ni ufunguo wa maisha,wekeza sasa kwa maendeleo ya Taifa letu.”** Jumbe nyingine zinazoambatana na Ujumbe mkuu wa mwenge wa Uhuru ni pamoja na ujumbe wa Mapambano dhini ya Rushwa unaosema **“Kataa rushwa –Jenga Tanzania”**, Ujumbe wa Mapambano dhidi ya UKIMWI unaosema **“Mwananchi Jitambue Pima Afya yako sasa”** Ujumbe wa mapambano dhini ya dawa za kulevya unaosema **“Tuwasikilize na kuwashauri watoto ili wasitumie Dawa za Kulevya”** ambapo ujumbe wa mapambano dhidi ya malaria unasema, **“Shiriki kutokomeza malaria kwa manufaa ya Jamii”**

Mwenge wa Uhuru utakimbizwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kwa muda wa siku moja ambapo utazindua na kuweka mawe ya msingi katika miradi 12 ya maendeleo iliyoko Katika kata

mbalimbali za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo. Baada ya shughuli ya uzinduzi wa Miradi, Mwenge wa Uhuru utakesha katika Uwanja wa Mpira Kanoge Laini ambapo kutakuwa na burudani mbalimbali zitakazotolewa na Wasanii, Bendi za Muziki na Vikundi mbalimbali vya ngoma.

Baada ya Mwenge wa Uhuru kukeshwa katika Uwanja wa Mpira Kanoge Laini utakabidhiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda Wilayani Tanganyika ili kuendelea na ratiba yake ya uzinduzi wa miradi mbalimbali ya Maendeleo Nchini.

Mkurugenzi Mtendaji kwa niaba ya watumishi wote pamoja na kamati mbalimbali za maandalizi anawatakiwa wananchi wote maandalizi mema ya tukio la kipekee la Mapokezi ya Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa kwa Mwaka 2018.

“Elimu ni ufunguo wa maisha, wekeza sasa kwa maendeleo ya Taifa letu.”

Imetolewa na :



John A. Mganga

Afisa Habari Mawasiliano na Uhusiano(W)

Kitengo cha Habari Mawasiliano TEHAMA na Uhusiano,

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.